Utangulizi Juu ya Kulinda Usalama dhidi ya Unyonyaji wa Kijinsia, Dhuluma na Unyanyasaji wa Kijinsia

Q&A

26 Oct 2021

Swali Kwanini Watu wengi kama unafanya Kazi ya Humanitarian as a component kwenye organization wanaonekana kama hawafanyi hizi kazi mpaka Kila component ihusiane na Humanitarian

Jibu: Kama nimekuelewa vizuri,Kwa uzoefu tu kulingana na swali lako mara nyingi mashirika yanayofanya kazi kwenye sekta ya misaada ni kama vile wanaofanya kwenye kambi za wakimbizi au waliokumbana na changamoto za mafuriko au kimbunga kikali.Kwa hiyo hata mambo wanayokumbana nayo ya kiusalama ni tofauti na mashirika yanayofanya kwenye Mazingira ya kawaida kama sekta za maendeleo.Kwa hiyo si kila shirika linalofanya kazi ya kusaidia watu au wanufaika wanafanya kazi kwenye sekta ya msaada.

Nini kifanyike pale imani za kimila zinapotofautiana na msimamo wa sheria? Mfano ukeketaji au ndoa za utotoni. Hii ni kwa sababu ukatili unaofanyika mara nyingi hata wahanga hawajui kama wanafanyiwa ukatili au hawaoni mazingira salama ya kutoa taarifa.

Jibu: Kweli katika jamii zetu za kiafrika bado kuna Imani za kimila na mambo mengine ya kiutamaduni yanayokinzana na sheria na kuleta madhara kwa Watoto au wanawake. Nchi husika zinatakiwa kuchukua hatua ya kuendelea kuelimisha jamii husika na kuendelea kuweka sheria zinazowabana wale wote wanaofanya vitendo vya kimila vyenye kuleta madhara kwa Watoto au wanawake au makundi mbalimbali yaliyoko kwenye jamii. Mfano Tanzania kwa kupitia sheria ya mtoto, 2009 na sheria ya makosa ya Jinai imezuia moja kwa moja vitendo vya ukeketaji

Kulipoti kwa watu ambao wana uzoefu - tunadumu kwa wakulima kuna mfano watu tunaoweza shirikiana nao

Jibu: Kama nakuelewa vizuri,kazi hizi za kulinda usalama zinahitaji zaidi ushirikiano na mashirika mengine na serikali kulingana na mazingira mnayofanyia kazi.Kwa Mfano kama shirika lenyu mnafanya kazi na wakulima ni kuangalia pia shughuli gani ambazo mnazifanya zinavyoweza kuathiri wakulima,inaweza kuwa sera zenu au programu au wafanyakazi.

Je kuna michakato gani ya kufanya mabadiliko ya sheria zetu za Tanzania ambazo mpaka sasa zinaonekana zimepitwa na wakati na zinamnyonya mtoto. kwa mfano sheria ya Ndoa, lakini pia sheria ya kupambana na ukeketaji na usafirishaji haramu wa Watoto

Jibu: Baadhi ya wadau kutoka asasi za kiraia nchini Tanzania wakiongozwa na Rebeca Gyumi walipeleka shauri la kufutwa kipengele kinachomruhusu mtoto wa kike kuolewa akiwa na umri wa miaka 15 ,shauri lilipelekwa Mahakama Kuu, na Mahakama kuu iliamua hicho kipengele kufutwa kwa kuwa kilipingana na katiba ya Jamhuri ya Muuungano wa Tanzania na kutoa muda wa serikali kufanya mabadiliko lakini hadi mabadiliko hayajafanyika lakini asasi za kiraia zinaendelea kufanya ushawishi ili hayo mabadiliko yatokee.

Kuhusu mazingira, mimi naona mazingira yanaweza kuanzia tangu nyumbani, shuleni, vyuoni na hata makazini. Lakini inawezekana kwamba mashirika/ofisi nyingi hawajazingatia "kulinda usalama"

Jibu : Ni kweli kabisa ukatili na vitendo vingine vya unyanyasaji vinafanyika mahali kokote kuanzia nyumbani hadi maofsini . Ili kuzuia ukatili unafanyika nyumbani ni vyema wazazi na jamii nzima kwa ujumla kuendelea kuelimishwa ukatili , na namna ya kuzuia na kushughulikia hivyo vitendo. Kwa ngazi ya Taasisi au mahali pa kazi ni vyema Taasisi zikaweka Sera ya kuzuia ukatili au vitendo vya udhuluma au unyonyanyi dhidi ya Watoto na watu wazima hususani walioko kwenye mazingira magumu au hatarishi. Baadhi ya asasi za kiraia zilishaweka utaratibu huo na nyingine zinaendelea kuweka. Tunahitaji kuendelea kujifunza kutoka kwa wale ambao wameishaweka utaratibu huo kwenye taasisi na kuangalia hizo sera zinafanyaje kazi.

Naitwa Ann. Je tutahuzisha mahakama zetu aje. Wakati mwingi mahakama husema hakuna ushaidi wa kutosha.

Jibu : Vitendo vya ukatili au unyonyaji au dhuluma vingine hufikishwa mahakamani na sheria zetu zinataka mahakama kabla haijatoa hukumu ipate Ushahidi wa kutosha . Na wakati mwingine wanajamii washindwa kutoa Ushahidi wa kutosha aidha kwa sababu ya kutoelewa au kutopata msaada mzuri wa kisheria . Hivyo basi ni jukumu la nchi husika kushirikiana na wadau au asasi za kiraia kuendelea kuelimisha jamii umuhimu wa kutoa taarifa na kuelewa umuhimu wa kutoa Ushahidi.

Pia asasi zinazoshughulika na wahanga wa vitendo vya ukatili au unyonyaji ziendelee kushirikiana na mahakama, jeshi la polisi kwa kukutana mara kwa mara na kubadilishana uzoefu, na kuweza kueleza changamoto zinazowakabili.

Swali langu ni kwa Martin,anasisitiza umuhimu wa kuhakikisha usalama ndani ya asasi,Muhanga tujue kuwa ili asaidike pia mifumo yanje nayo inahusika sana. Mifumo hii ndiyo inachangia sana kuvunja na kuchochea ukatili badala ya kusaidia. Nini ushauri wako

Jibu: Ni kweli kabisa shiriks linaweza kuwa linahakikisha usalama,na kutambua kesi lakini mifumo ikakandamiza wahanga.Mfano kesi ikiripotiwa polisi au ustawi wa jamii lakini wasisshughulike kwa makini na kusababisha wahanga/waathirika kuendelea kuumia.Nakubaliana na wewe kabisa kwamba kulinda usalama si swala tu la shirika tu ni kazi la mifumo inayotunguka pia.

Hongereni sana kwa uwasilishaji mzuri, katika kuwasaidia wahanga waliopitia vitendo vya unyanyasaji/ukatili, mara nyingi unakuta msaada wa haraka unatoka ni wa kisheria, je kuna uwezekano wa kuangalia namna ya kusaidia survivors on dealing with experienced trauma as a first track support ili wajisikie wana utu na thamani na kuweza kutoa ushirikiano Zaidi.

Jibu: Ni kweli ni muhimu sana kuangalia namna ya kuweka mipango yetu ili wahanga wasiishie kupata msaada wa kisheria tu.Maana msaada kwa mhango unatakiwa kutolewa kulingana na namna alivyoathirika na hasa kuangalia Athari mbalimbali.Hii inatufundisha sisi wadau Kuhakikisha tunatathimini Athari za mhanga kwa kuangalia ukubwa wa tatizo na kuangalia kwa kiwango gani ameathirika kisaikolojia.,kimwili na kijamii.

Nadhani uwepo wa sera ya Kulinda usalama, unaleta haja ya uwepo wa wanasheria katika ofisi zetu za kazi

Jibu: Nakubaliana na wewe kabisa juhudi za kulinda usalama zinahitaji wadau wengi ikiwemo wanasheria ambao hutoa ushauri pale suala linapokuwa linahitaji utatuzi wa kisheria ; au kuelimisha wafanyakazi juu ya sheria zinazohusu masuala ya ukatili , unyonyaji na dhuluma. Hivyo basi ni vyema shirika au taasisi zikawa na afisa sheria mahala pa kazi au zikishindwa kuwa naye permanent ni vyema zikajitahidi kufanya kazi karibu sana na zile taasisi zinazotoa msaada wa sheria ili kuweza kupata miongozo mbalimbali wakati wakishughulika na wahanga wanaohitaji msaada wa sheria.

Je ni njia gani nzuri zitakazoweza kuleta mabadiliko ya sheria ya ndoa ikiwa viongozi wa serikali hawataki kukubali kufanya mabadiliko?

Jibu :Ni vyema majadiliano yakaendelea kufanyika kati ya asasi na viongozi wa ngazi za juu; au kuziomba kamati za kimataifa kuendelea kutoa ushauri na mapendekezo juu ya hilo suala.

Licha ya uwepo wa sera zinahusika na kuwalinda walengwa, lakn wakati mwingine ni vigumu kwa mhanga kutoa taarifa au ripoti ya kunyanyasika. Je, kipi cha weza kufanyika ili kuhamasisha walengwa au wahanga kutoa taarifa

Jibu: Wahanga wanatakiwa kujenga uwezo wa umuhimu wa kutoa utaarifa, lakini kuhakikishiwa usalama wao wanapotoa taaarifa . Hivyo shirika linapotunga sera ya kulinda usalama lihakikishe pia linaweka msisitizo kwenye kanuni ya usiri , lakini pia na kuweka sera ya kulinda usalama mpiga filimbi (Whistle blowing Policy).

Panapotokea mfanyakazi ametokea kuwa na mahusiano ya kimapenzi na mdau wa kikazi na wanania ya ndoa hii itakuwa ni sehemu ya safegurading na ni halali?

Jibu: Kama watu wazima ambao ni wafanyakazi(wenyewe kwa wenyewe) wakaamua kuweka mahusiano kwa hiari yao na wana nia ya kuoana hiyo sio Safeguarding; lakini kwa nia ya kuleta ufanisi katika kazi na kuhakikisha hakuna favourism au upendeleo hao wanatakiwa kutoa tu taarifa kwa Afisa Raslimali (Human Resource) wa Shirika (yeye ndio ataangaalia hayo mahusiano yana athari gani kwenye kazi au shirika.

Kama ni mahusiano kati ya mtoa huduma/mfanyakazi na anayepokea huduma mara nyingi sera na miongozo mbalimbali ya kimataifa, na baadhi ya maadili ya tasisi husika yanakataza na hii ni kwa nia ya kumlinda huyo anayepokea huduma kwani watoa huduma wanaweza wakatumia mamlaka yao kuwaingiza watoa huduma kwenye mahusiano au mpokea huduma anaweza kukubali mahusiano kwa vile anamuogopa mtoa huduma. Ni vyema taasisi ikaweka sera au taratibu ya kuratibu mahusiano ya kimapenzi baina ya mfanyakazi na mfanyakazi ; pia baina ya mfanyakazi na mpokea huduma.

Licha ya uwepo wa sera zinahusika na kuwalinda walengwa, lakn wakati mwingine ni vigumu kwa mhanga kutoa taarifa au ripoti ya kunyanyasika. Je, kipi cha weza kufanyika ili kuhamasisha walengwa au wahanga kutoa taarifa(hili liko sawa na swali namba 11